

MKAKATI DHIDI YAWALA RUSHWA NA MAFISADI AFRIKA MASHARIKI WAIVA

Na Mussa Misalaba, Arusha

Septemba 19, 2018

Kazi ya kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi kwenye ukanda wa Afrika Mashariki kwa kipindi cha 2019 - 2023 imekamilika kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali.

Kauli hii imetolewa tarehe 18 Septemba, 2018 na Kaimu Mwenyekiti wa Umoja wa Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki (EAAACA), Wedo Atto, kwenye ufunguzi wa Mkutano Mkuu Maalumu wa viongozi wa umoja huu unaofanyika jijini Arusha kwa siku tano kati ya Septemba 18 na 21, 2018.

Katika ufafanuzi wake, Kaimu mwenyekiti wa umoja huu alisema:

“Kutokana na mabadiliko ya mwenendo wa makosa ya rushwa duniani EAAACA imekuja na mpango mkakati wa miaka mitano wa mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi unaolenga kuimarisha, kuunda na kuwa na programu za kipaumbele na mitandao muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi”.

Programu za kipaumbele ni pamoja na uendeshaji wa mafunzo ya pamoja ambapo watumishi kutoka taasisi wanachama watapatiwa mafunzo mbalimbali ya weledi yatakayowawezesha kutekekeleza majukumu yao ya kuzuia na kupambana na rushwa katika nchi zao.

Kutokana na mpango mkakati huu, EAAACA ina kusudia kuimarisha na kupanua mitandao yenye manufaa mathalani ya kubadilishana taarifa na

kusaidiana katika ufuatiliaji na urejeshaji wa mali zilizotoroshewa nje ya nchi na waharifu wa makosa ya rushwa na uufisadi ndani ya ukanda wa nchi za Afrika Mashariki.

“Hatuna budi kuuimarisha mtandao wetu wa ufuatiliaji na urejeshaji mali iliyotoroshwa ndani ya umoja wetu (ARIN- EA) ambao umekuwa na mafanikio makubwa toka mwaka 2013 tulipouanzisha”, alisisitiza Kaimu mwenyekiti wa umoja huu.

Mbali na uimarishaji wa mtandao wa ARIN- EA, Kaimu mwenyekiti wa umoja huu alisema mpango mkakati huu unabainisha maeneo ya kimkakati katika ushirikiano na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya rushwa na uufisadi ndani na nje ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa chini ya mwavuli wa EAAACA ni pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU (Tanzania), Tume ya Maadili na Vita dhidi ya Rushwa – EACC (Kenya), na IG (Uganda),

Zingine ni Ofisi inayoshughulikia Kero - Ombudsman (Rwanda), Brigade Maalumu ya Kupambana na Rushwa (Burundi), Tume ya Kupambana na Rushwa Sudani Kusini – SSACC (Sudan Kusini), FEACC (Ethiopia) na Brigedi Maalumu dhidi ya Rushwa (Djibouti).

Umoja wa Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki ulianzishwa Septemba 8, 2007 jijini Kampala Uganda ambapo TAKUKURU, EACC na IG zilihusika na baadaye mamlaka zingine nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki zilijiunga.